



NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL (NEMC)

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi mkuu, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), anawatangazia wawekezaji wote kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, Kifungu cha 81 na Kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira ya Mwaka 2005, Miradi yote inatakiwa kuwa na cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) au Cheti cha Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*). Miradi hiyo ni pamoja na: -

- i. Majengo yenye ghorofa zaidi ya 3;
- ii. Majengo ya Biashara, Ofisi na Hoteli;
- iii. Viwanda vyote;
- iv. Maduka Makubwa (*Super Markets, Shopping Malls*);
- v. Vituo vya Mafuta (fuel filling, service stations and *fuel depots*);
- vi. Miradi ya Uchimbaji na Uchenjuaji Madini;
- vii. Maghala (Warehouses), na;
- viii. Mashamba makubwa ya miti, Kilimo na Mifugo;

Kutokuwa na cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) au Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*) kwa miradi hiyo ni kosa kisheria na utachukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kufungiwa shughuli zako.

Kwa hiyo, Baraza linawakumbusha wenye miradi wote kuwa, lazima miradi iliyotajwa kwenye Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 ifanyiwe Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) au Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*) na kupata cheti cha Mazingira. Kutofanya hivyo ni kutenda kosa kwa mujibu wa kifungu Na. 81 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004.

Kama huna cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) au Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*), Baraza **LINAKUTAKA** kusajili mradi wako kwenye ofisi za Baraza Makao Makuu, Mtaa wa Migombani Mikocheni Dar es Salaam. Au, unaweza kusajili katika Ofisi za Kanda zilizopo Mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza ili kupata cheti hicho. Baraza linawataka kufanya hivyo maramoja, kutakuwapo na ukaguzi wa kina kutathmini utekelezaji wa agizo hili.

Aidha, Baraza linawakumbusha watu wote kulipa ada ya mazingira ya mwaka kwa mujibu wa sheria ya Mazingira, 2004. Pia, **Wataalam Washauri wa Mazingira** (*Environmental Experts*) na makampuni ya washauri wa mazingira (*Firms of Environmental Experts*) wanakumbushwa kulipa ada ya mwaka bila kukosa. Kutofanya hivyo, ni kuvunja sheria na hatua kali zitachukuliwa ikiwemo kufutiwa usajili.

Kwa maelezo zaidi piga namba: **0754584260/ 0715511561.**
0692108566-dawati la malalamiko na msaada

Taarifa imetolewa na ;
Ofisi ya Mkurugenzi MKuu,
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),
35 Regent Street, S.L.P 63154, 11404 Dar es Salaam